



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**



**RATIBA YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**  
**(STANDARD FOUR NATIONAL ASSESSMENT TIMETABLE)**  
**OKTOBA, 2023**

TAREHE NA SIKU	MUDA (SAA)	NAMBA MFICHO	SOMO
<b>25.10.2023</b> <b>JUMATANO</b>	2:00 – 3:30	01	KISWAHILI
	<b>3:30 – 4:30</b>		<b>MAPUMZIKO</b>
	4:30 – 6:00	04 04E	HISABATI MATHEMATICS
	<b>6:00 – 8:00</b>		<b>MAPUMZIKO</b>
	8:00 – 9:30	03 03E	MAARIFA YA JAMII SOCIAL STUDIES
<hr/>			
<b>26.10.2023</b> <b>ALHAMISI</b>	2:00 – 3:30	05 05E	SAYANSI NA TEKNOLOJIA SCIENCE AND TECHNOLOGY
	<b>3:30 – 4:30</b>		<b>MAPUMZIKO</b>
	4:30 – 6:00	02	ENGLISH LANGUAGE
	<b>6:00 – 8:00</b>		<b>MAPUMZIKO</b>
	8:00 – 9:30	06 06E	URAI NA MAADILI CIVIC AND MORAL EDUCATION

## MAELEKEZO MUHIMU

1. Hakikisha kuwa unayo **Ratiba ya Upimaji wa mwaka 2023** iliyoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.
2. **Kabla ya kufungua bahasha** yoyote yenye maswali ya upimaji, hakikisha kwamba **unasoma jina la somo juu ya bahasha husika** na kujihakikishia kuwa somo hilo ndilo linalostahili kufanyika wakati huo kulingana na **Ratiba ya Upimaji**.
3. Endapo utata utajitokeza kati ya **maelekezo yaliyomo katika Karatasi ya Upimaji na Ratiba ya Upimaji, maelekezo yaliyomo katika karatasi ya upimaji husika ndiyo yatakayofuatwa**.
4. Wanafunzi wenye mahitaji Maalum (**Wasioona, Uoni hafifu, Viziwi**) waongezewe **MUDA WA ZIADA WA DAKIKA 20 KWA KILA SAA** kwa somo la **Hisabati** na **DAKIKA 10 KWA KILA SAA** kwa masomo mengine.
5. Msimamizi wa wanafunzi wenye **mahitaji maalum** awe **Mtaalamu** mwaminifu wa mahitaji husika.
6. Wanafunzi wenye **UONI HAFIFU** wapewe karatasi za upimaji zenye **maandishi yaliyokuzwa**, zilizoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa matumizi yao.
7. Wanafunzi waelekezwe;
  - (a) Kuingia ndani ya chumba cha upimaji nusu saa kabla ya muda wa upimaji na watakochelewa kwa zaidi ya nusu saa baada ya upimaji kuanza hawataruhusiwa.
  - (b) Kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na wasimamizi wa upimaji.
  - (c) Kuandika jina kamili na namba ya upimaji kwa usahihi.
  - (d) Kutofanya mawasiliano ya maneno au kwa njia yoyote baina yao. Ikiwa mwanafunzi ana tatizo anatakiwa kunyoosha mkono ili kuomba msaada kwa msimamizi wa upimaji.
  - (e) Watakojihusisha au watakaofanya udanganyifu watafutiwa matokeo yao ya upimaji.